***HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA***

# ***SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ZA MWAKA 2013***

**TANGAZO LA SERIKALI NAMBA 364 LA TAREHE 03/10/2014**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI), 1982**

**(SURA YA 288)**

**SHERIA NDOGO**

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 89(1)*

**SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA ZA MWAKA 2013**

| | | |
|---|---|---|
| Jina na mwanzo wa kuanza kutumika | 1 | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za mwaka 2013 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| Matumizi | 2 | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. |
| Tafsiri | 3 | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapohitajika vinginevyo:- |

"Ada ya kuondoa taka" ina maana ya kiwango cha fedha kilichowekwa na Halmashauri kulipia gharama za kuzoa taka kama ilivyochanganuliwa kwenye Jedwali na. 1;

"Adha" maana yake ni kitu chochote ambacho kimewekwa au kujengwa katika hali ya uchafu na kinaweza kusababisha:-

a) Madhara kwa maisha ya binadamu, wanyama au kiungo chake;
b) Chenye kuleta maudhi; au
c) Kitu chochote kinachoweza kusababisha magonjwa.

"CBO" (Comunity Based Organisation), maana yake ni kikundi cha jamii kilichoundwa kwa ajili ya kutatua tatizo au kufanya shughuli za maendeleo katika jamii ya eneo hilo ambapo CBO imeundwa;

"Eneo lililozuiwa "maana yake ni maeneo yote yaliyoko chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ambapo majani marefu na mimea imepigwa marufuku kuwepo na inahusisha maeneo ya wazi, mitaa na barabara;

"Huduma" maana yake ni kusafisha, kuondoa, kukusanya na kutupa taka za barabarani, maeneo ya wazi, nyumba za kuishi, nyumba za biashara na kuzibua mitaro ya maji ya mvua;

"Kampuni" maana yake ni kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za makampuni na inajishughulisha na huduma za usafi wa mazingira;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ;

"Kaya" maana yake ni familia ya baba na mama, watoto na wategemezi;

"Kuzuia" maana yake ni kitendo kinachofanywa na mtu kwa kutazamia au kuashiria kukataza moja kwa moja mtu ambaye amepewa mamlaka na Halmashauri kutekeleza Sheria Ndogo hizi aidha kwa kutumia nguvu au vitisho;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela pamoja na anayekaimu;

"Mzabuni" maana yake ni mtu au kikundi cha watu au kampuni iliyoidhinishwa na Halmashauri kufanya kazi zozote kama atakavyoelekezwa na Halmashauri kwa niaba yake;

"Mahakama" maana yake ni mahakama ya ngazi yoyote na italihusisha pia Baraza la kata;

"Majani" maana yake ni majani au vichaka vyenye urefu wa sm 20 au zaidi vilivyopo maeneo yaliyokatazwa.

"Maji taka" maana yake ni kinyesi au mkojo na uchafu

mwingine kama maji ya kuoga na maji ya kupigia deki, kuosha vyombo, maji yanayotokana na uchafu kutoka vituo vya mafuta, vituo vya kuoshea magari na viwandani ambapo yana kemikali au yasiyokuwa na kemikali na ambayo hayajasafishwa;

"Mtaa" inajumuisha barabara yeyote ndogo au kubwa au njia ya kupita kwa miguu au barabara nyembamba ya kufanya usafi au ya kwenda kwa miguu ipitayo kwenye maeneo ya wazi ambayo inatumiwa na jamii na pia inajumuisha daraja lipitalo juu ya barabara au njia;

"Mkazi mmiliki" inajumuisha mtu yeyote aliyetwaa na kumiliki eneo au nyumba ya kuishi au nyumba ya biashara bila kujali jina au cheo anachotumia mmiliki na kuwa mpangaji wa nyumba ya kulala hata kama amepanga chumba kimoja au hata kama wako wapangaji wengi;

"Makazi" maana yake ni nyumba, ghorofa au jengo lolote linalotumiwa kwa kuishi, pia inajumuisha ardhi ambayo haijaendelezwa lakini imetolewa au imetengwa kwa ajili ya nyumba za kuishi;

"Nyumba" maana yake ni jengo la aina yoyote lililojengwa na linajumuisha nyumba za makazi na nyumba za biashara;

"Premises" inajumuisha ardhi, majengo, magari, mabehewa ya reli na vyombo vingine vya kubebea, mahema, mikokoteni, gari la mizigo, ujenzi wa aina yeyote, mifereji, maziwa na bahari, ufuko, bomba la maji au eneo lolote liwe wazi au limefunikwa au liwe limeendelezwa au bado kisheria, pia meli mashua ama mitumbwi, winchi au chombo chochote cha majini kitakachokuwa kwenye bwawa, ziwa, mto, barabara au katika eneo lolote la Halmasahuri;

"Wakala" ina maana ya mzabuni aliyeteuliwa na Halmashauri kutoa huduma zinazohusiana na udhibiti wa taka ngumu au maji taka kwa niaba yake;

"Taka ngumu" maana yake ni takataka zote zinazo zalishwa majumbani, kwenye taasisi, maeneo ya biashara, viwandani pamoja na takataka zote zinazozalishwa mahali popote zisipostahili, mizoga, magari mabovu lakini

haihushi maji taka;

"Sewer" (bomba kuu la maji taka) ni mtandao wa mabomba kwa ajili ya kusafirisha maji taka kutoka katika nyumba au sehemu nyingine ya maji taka yanapozalishwa;

"Soko" ina maana ya soko lililowekwa na Halmashauri kisheria au eneo ambalo linatambulika kisheria na Halmashauri la kufanyia shughuli za biashara;

"Taka za majumbani" maana yake ni taka za kawaida zilizozalishwa kwenye nyumba za kuishi;

"Taka za biashara" ina maana taka zote zile zitokazo kwenye maeneo ya biashara au viwandani kwa kuzalishwa na viwanda vyenyewe au wakati huduma zinapotolewa ambazo sio kwenye makazi ya watu pia hujumuisha taka nyingine zote ambazo sio za majumbani.

"Taka hatarishi" maana yake ni taka zenye sumu, taka zinazoweza kuwaka moto, taka zinazoweza kula mwili au vyuma, taka zenye mionzi ya kurutubisha (radioactive), taka zinazoweza kulipuka au taka zilizo hatari kama ilivyobainishwa na taasisi ya kulinda mazingira ya Tanzania (Tanzania Environment Protection Agency) inajumuisha mafuta ya dizeli, mafuta ya taa, petroli, rangi, mafuta ya kuyeyushia (solvent), betri za tochi, betri za magari, madawa ya kuulia wadudu waharibifu na taka za hospitali au zinazoambukiza maradhi kutoka hospitali na zahanati, mafuta mazito ya kuteleza na mafuta ya kulainisha na kuchanganya na vitu vingine kutoka kwenye viwanda, asbesto, mizoga au maiti;

Ukaguzi wa maeneo ya Manispaa

4 (1) Afisa yeyote aliyeidhinishwa na Halmashauri atakuwa na uwezo wa kukagua eneo lolote lililopo chini ya mamlaka ya Halmashauri kwa nia ya kuangalia adha na kutoa maelekezo ya kuondoa adha hizo.

(2) Maafisa hao ni Mkurugenzi pamoja na watendaji wake inajumuisha pia wenyejiviti na watendaji wa kata na Mitaa.

Utupaji taka ovyo

5 (1) Ni marufuku mtu yeyote kuweka au kutupa taka, mchanga au uchafu wowote utakaoleta chukizo katika mtaa,

uchochoro au eneo lolote lililokatazwa na Halmashauri.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa kinyesi, mkojo, mate au matapishi katika uchochoro, mtaa au eneo lolote lisiloruhusiwa.

(3) Itakuwa ni kosa kukiuka au kwenda kinyume na kifungu cha 5 (1) na (2) cha Sheria Ndogo hizi.

Vifaa vya kukusanyia taka

6 (1) Mtu yeyote anayemiliki nyumba au mpangaji anatakiwa kuweka chombo cha kukusanyia taka chenye ukubwa unaotosheleza na kiwe na mfuniko unaofaa na kinatakiwa kitumike kila siku katika nyumba hiyo.

(2) Kulingana na kifungu kidogo cha (1) cha Sheria Ndogo hii ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka katika chombo cha kuhifadhia taka au maji machafu kitu chochote ambacho kinaweza kuleta madhara kwa binadamu au kusababisha moto au magonjwa.

(3) Takataka zote zihifadhiwe ndani ya vyombo vya kuhidhia taka mpaka hapo zitakapochukuliwa na Halmashauri au mwenye nyumba au mpangaji na kuzipeleka mwenyewe kwenye maeneo maalumu yaliyotengwa.

(4) Mmiliki wa nyumba au mpangaji wa nyumba atalazimika kutunza takataka zilizohifadhiwa kwenye pipa la taka au chombo chochote kinachokubalika kisheria hadi hapo Halmashauri au mtu yeyote aliyeteuliwa na Halmashauri atakapozichukua na kuzitupa kwenye eneo maalumu lililotengwa.

(5) Ukusanyaji wa taka ngumu unaofanywa na Halmashauri au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Halmashauri kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Halmashauri atakuwa na uwezo wa kutoza ada ya uzoaji wa taka hizo na ada hiyo itatozwa kama ilivyo orodheshwa katika Jedwali na. 1 la Sheria Ndogo hizi.

(6) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kukiuka matakwa ya kifungu hiki cha 6 na atiwapo hatiani atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu hamsini au kwenda kutumikia kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Wajibu wa kutunza mazingira

7 (1) Ni jukumu la mwenye nyumba au mpangaji kuweka chombo cha kuhifadhia taka katika nyumba yake ili kuwezesha ukusanyaji wa taka hizo kuwa urahisi.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukojoa, kujisaidia haja kubwa, kutupa maganda ya miwa, maganda ya ndizi au kitu chochote katika barabara, sehemu ya wazi au sehemu yoyote isiyoruhusiwa.

Wajibu kwa wamiliki au wasimamizi wa magari ya abiria

8 (1) Kila mwenye basi litakaloingia eneo la Manispaa na wenye magari ya abiria mjini (express), atawajibika kuwa na chombo cha kuhifadhia taka na kuhakikisha kwamba kila abiria anatupa taka ndani ya chombo hicho.

(2) Itakuwa ni kosa kwa mwenye basi au dereva au kondakta iwapo abiria aliyeko ndani ya basi lake atatupa kitu chochote barabarani au stendi.

(3) Mwenye basi au dereva au kondakta atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu hamsini baada ya kujaziwa fomu ya ilani na afisa muidhiniwa wa Manispaa endapo abiria aliyeko ndani ya gari lake atatupa uchafu katika barabara au kituo cha mabasi.

Utupaji taka kwenye barabara au sehemu za wazi

9 (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumwaga takataka ovyo barabarani, kando ya barabara, kwenye mitaro ya maji ya mvua, sehemu za wazi na maeneo ya kuzunguka makazi.

(2) Ni marufuku kuchoma takataka ovyo bila idhini ya Halmashauri.

Wajibu wa Kutunza uzio

10 Mwenye nyumba au mpangaji anatakiwa kukata majani yaliyozidi kimo cha sm 20 na kukata uzio na kuondoa mabaki na kuyaweka kwenye chombo cha kuhifadhia taka au sehemu iliyoruhusiwa kuhifadhi taka hizo.

Murufuku kumwaga maji taka ovyo

11 Ni marufuku mtu yeyote kumwaga, kutiririsha maji taka katika mtaa, uchochoro, eneo la wazi, mitaro ya maji ya mvua, au eneo lolote lisiloruhusiwa.

Wajibu wa kuelekeza maji taka kwenye mfumo rasmi

12 Utakuwa ni wajibu wa mwenye nyumba kuunganisha choo cha maji na uchafu wake kwenye mfereji mkuu wa maji taka pale ambapo kuna mfumo, eneo ambapo hakuna mfumo wa majitaka, mwenye nyumba atatakiwa aelekeze uchafu huo katika mashimo ya maji taka yaliyokubaliwa na Halmashauri kwa kulingana na maelekezo yaliyopo kwenye kibali cha ujenzi.

Marufuku ya uchafuzi wa maji

13 (1) Ni marufuku mtu yeyote kuchafua au kuvuruga maji yanayotumika kwa matumizi ya binadamu au wanyama.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kuoga na kufulia kwenye chanzo cha maji, ziwa, mto, kisima au tanki ambalo halikuwekwa kwa madhumuni hayo.

Kuzuia adha ya maji taka katika nyumba za kupanga

14 Endapo kutatokea adha zinazosababishwa na maji taka katika nyumba yenye mpangaji zaidi ya mmoja na iwapo mwenye nyumba hawezi kupatikana kwa haraka, Halmashauri inaweza kuamuru wapangaji kufanya lolote linalowezekana ili kuondoa kero hiyo na gharama hizo zitafidiwa na kodi watakayomlipa mwenye nyumba.

Wajibu wa kujenga vyoo

15 (1) Mtu yeyote anayemiliki jengo au nyumba inayotumika kama makazi, anatakiwa aweke vyoo vya kutosha kama Halmashauri itakavyoona inafaa.

(2) Mtu yeyote anaye miliki kiwanda, shule, mgahawa, shule za bweni, hoteli au jengo lolote la umma, sehemu za burudani au nyumba yoyote atatakiwa kuweka vyoo vinavyoridhisha kwa ajili ya matumizi ya wanaume na

wanawake na atahakikisha kuwa vyoo hivyo vina mwanga na hewa ya kutosha.

(3) Ni marufuku mtu yeyote kuendesha biashara ya nyumba ya wageni au hostel ya wanafunzi bila ya kibali cha Halmashauri.

(4) Kila mgahawa wa vyakula au vinywaji lazima pawepo na vyoo vya kutosha kwa ajili ya wateja, watumishi na wapita njia.

(5) Kila mwenye hoteli, mgahawa, nyumba ya kulala wageni, kiwanda, karakakana, café na magenge ya vyakula yaliyoruhusiwa atatakiwa kuhakikisha anapima Afya za wafanyakazi wake kwenye hospitali ya serikali kila baada ya miezi sita na atalipa ada kama ilivyooneshwa katika Jedwali namba 4 katika Sheria Ndogo hizi na Halmashauri itatoa cheti maalumu kwa waliopima afya ili kudhibiti maambukizi ya magonjwa.

(6) Choo cha aina yoyote ambacho kwa maoni ya Halmashauri kitaonekana kichafu au kuhatarisha maisha ya binadamu, hakitaruhusiwa kutumika mpaka hapo Halmashauri itakaporidhika na matengenezo yaliyofanyika.

(7) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba au kujenga shimo kwa ajili ya kuhifadhi kinyesi au maji taka bila idhini ya maandishi iliyotokewa na Halmashauri.

Wajibu wa kiwanda kusafishia majitaka

16 (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha kiwanda chochote kinachotoa maji taka bila kuwa na mitambo ya kusafishia maji taka hayo ambayo imeidhinishwa na Halmashauri.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kuruhusu maji taka kutoka kiwandani au eneo lolote linalofanya utengenezaji kuingia katika vyanzo vya maji safi, ardhini, maeneo ya wazi, mitambo ya majitaka, uchochoro, mitaro iliyowazi kabla ya kuyasafisha kwa kiwango kinachokubalika na Halmashauri.

(3) Kila baada ya miezi mitatu kabla na baada ya kuyasafisha maji taka kutoka viwandani yatatakiwa kupimwa ili kuangaliwa ubora wake na maabara ya serikali au maabara yoyote iliyoruhusishwa na serikali na majibu au

matokeo ya uchunguzi huo kuwasilishwa Halmashauri.

Wajibu wa kutunza usafi wa eneo linalo zunguka nyumba

17 (1) Ni marufuku mtu yeyote kusababisha au kuruhusu eneo la nyumba anayoishi kuwa na uchafu wa takataka ya aina yoyote.

(2) Itakuwa ni wajibu wa mmiliki/mpangaji wa nyumba kufagia na kuondoa uchafu au marundo ya uchafu na kuweka safi eneo lote la nyumba yake.

(3) Vichochoro vyote vitatunzwa na wenye nyumba husika na kila mwenye nyumba/ mpangaji atawajibika kutunza eneo lake yaani hatua za upande wake baada ya vigingi vinavyotenganisha viwanja katika uchochoro huo kwa mujibu wa sheria.

Adha zitokanazo na magari

18 (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutelekeza magari mabovu kwenye njia ya miguu, mitaa au vichochoro au mitaro iliyo wazi na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kutengenezea/kurekebishia gari au mtambo eneo ambalo sio mahususi kwa shughuli hiyo au eneo lisiloruhusiwa na Halmashauri.

(3) Ni marufuku mtu yeyote kuosha magari katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.

Uwezo wa kusismamia usafi

19 (1) Halmashauri au mtu yeyote aliyeteuliwa kuwa wakala atakuwa na uwezo wa kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha na kutupa taka za majumbani na taka za biashara kwa kutoza ada kama ilivyoainishwa katika Jedwali na.1.

(2) Kamati za maendeleo za mitaa na kata zitakuwa na uwezo chini ya Sheria Ndogo hizi kusimamia usafi kwenye maeneo yao kwa kukomesha utupaji taka ovyo na usafishaji wa vichochoro.

(3) Kamati za maenedeleo za kata na mitaa zitakuwa na uwezo wa kumtoza mtu yeyote atakayechafua mazingira kwa namna yoyote ile, faini isiyozidi shilingi elfu hamsini.

(4) Kamati za maendeleo za kata na mitaa zitakuwa na uwezo wa kuunda vikosi kazi vya kudhibiti uchafuzi wa mazingira kwa kushirikiana na kamati za Afya za kata au

mtaa.

(5) Iwapo mchafuzi wa mazingira hana fedha ya kulipa pindi anapokamatwa, kamati husika itawajibika kukamata mali yake yoyote yenye thamani sawa na faini hiyo.

(6) Fedha zitakazopatikana kwa njia hii zitatumika kwenye shughuli za maendeleo za mtaa au kata husika kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 19(8) na ni lazima zikatiwe stakabadhi rasmi itakayotolewa na Halmashauri.

(7) Kama mchafuzi hana fedha wala mali apewe adhabu ya kufanya usafi kwa kadri mamlaka/kata/mtaa utakavyoona inafaa.

(8) Kamati ya maendeleo ya kata au mtaa inaweza kuunda kikosi kazi katika mtaa au kata kwa ajili ya kudhibiti uchafuzi wa mtaa. Fedha inayopatikana kutokana na kazi hii itakatiwa stakabadhi na kikosi kazi kitalipwa asilimia 70% ya fedha iliyokusanywa. Asilimia 15% kati ya fedha itakayobaki itatumika kwa maendeleo ya kata au mtaa na 15% nyingine itawasilishwa Halmashauri kwa ajili ya gharama za uchapishaji wa stakabadhi;

(9) Kila mkazi au mwananchi atakuwa na uwezo wa kukamata au kutoa taarifa kwenye kikosi kazi, mtaa, kata au mamlaka kuhusu mtu yeyote anayefanya uchafuzi katika mtaa husika kwa makusudi. Endapo uongozi wa kikosi kazi, mtaa, kata kwa kushirikiana na Afisa muidhiniwa wataridhika na kushuhudia uchafuzi huo, mtuhumiwa atatozwa faini isiyozidi elfu hamsini na aliyetoa taarifa au kukamata mchafuzi atalipwa kutokana na faini hiyo kama ilivyofafanuliwa katika kifungu cha 19(8).

(10) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumzuia mjumbe wa kamati ya maendeleo ya kata au mtaa kutimiza matakwa ya Sheria Ndogo hizi.

Vifaa vya kutunzia taka katika nyumba za makazi na biashara

20 (1) Kila mkazi kwenye nyumba au mpangaji kwenye nyumba ya makazi atawajibika kuweka chombo cha kuridhisha cha kuweka taka za majumbani chenye ujazo unaoridhisha na chenye mfuniko unaofaa na kuhakikisha kuwa takataka zote zinazozalishwa kwenye nyumba hiyo zinawekwa humo kila siku.

(2) Kila mkazi kwenye nyumba ya biashara au mpangaji atalazimika kuweka chombo cha kuridhisha cha kuhifadhia taka za biashara chenye ujazo wa kuridhisha na mfuniko wa kubana na kuhakikisha kuwa taka zote zinazozalishwa zinawekwa kwenye chombo hicho na ujazo wake utosheleze kwa siku.

(3) Halmashauri kama itakavyoona inafaa itaelekeza sifa za chombo na ujazo wake utosheleze kwa siku.

(4) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kukiuka matakwa ya kifungu kidogo cha 20 (1) na atiwapo hatiani atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu hamsini au kwenda gerezani kwa kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Utunzaji na uondoaji wa taka za viwandani na taka za hospitali

21 (1) Kila mwenye biashara au mtumiaji wa sehemu ambapo taka za viwandani zinazalishwa kwa marundo au taka za hospitali, atapaswa kuzitunza taka hizo na kuhakikisha kuwa anaziondoa kwa usanifu wa kuridhisha au jinsi atakavyoelekezwa mara kwa mara na Halmashauri.

(2) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji wa taka hatarishi kwa biashara zote kulingana na ukubwa wa uzalishaji, au Halmashauri chini ya usimamizi wa Afisa muidhiniwa itamuamuru mwenye taka hatarishi kuziondoa na kuzitupa kadri Halmashauri itakavyoona inafaa.

(3) Mtu yeyote atayevunja sheria ndogo hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika, atapewa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000) au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja, kifungo na faini, pia atatakiwa kurejesha gharama za uharibifu atakaokuwa amesababisha.

Wajibu wa kuweka taka sehemu rasimi

22 (1) Kila mmiliki / mkazi wa nyumba ya makazi au nyumba ya biashara atawajibika kuweka taka zote azalishazo mahali atakapoelekezwa na Halmashauri, iwapo mtu yoyote atashindwa kufanya hivyo atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu yeyote atakayevunja sheria ndogo hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika ametenda kosa atapigwa faini isiyozidi elfu hamsini (50,000) au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kifungo na faini.

Mipango na utaratibu wa ukusanyaji na utupaji taka

23 (1) Halmashauri itaweka mipango na utaratibu wa ukusanyaji na utupaji taka kutoka kwenye sehemu za wazi, biashara, masoko na nyumba za kuishi na kuzizoa taka hizo na kuzitupa.

(2) Halmashauri inaweza kufanya kazi ya kukusanya taka yenyewe au kuteua wakala kwa makubaliano maalumu;

(3) Halmashauri imeutenga mji katika kanda nne za ukusanyaji, uzoaji na utupaji wa taka ngumu: Kanda I – Kata ya Kirumba. Kanda II – Kata za Nyakato A & B, Nyamanoro, Kitangiri, na Pasiansi. Kanda ya III – Kata za Ilemela, na Buswelu. Kanda IV – Kata za Bugogwa na Sangabuye.

Wajibu wa kukusanya na kuhifadhi uchafu utokanao na mifugo

24 (1) Kila mfugaji wa ng'ombe, mbuzi, kuku, nguruwe na wanyama wengine wa nyumbani atawajibika kukusanya na kuhifadhi uchafu wowote utokanao na wanyama hao kama vile kinyesi, manyoya, na uchafu utokanao na ufugaji huo mfano nyasi au mabaki ya vyakula vyao katika hali ambayo itairidhisha Halmashauri na ambayo haitaleta adha kwa jamii.

(2) Kila atakayetaka kufuga wanyama waliotajwa kwenye kifungu kidogo cha (1) cha Sheria Ndogo hii ni lazima awe na eneo la kutosha na atapewa kibali na Halmashauri.

(3) Hairuhusiwi kabisa ufugaji wa wanyama kwenye kifungu kidogo cha (1) cha Sheria Ndogo hii kwenye eneo la msongamano wa makazi.

(4) Kwa namna yoyote ile ufugaji ni lazima uwe wa mnyama au ndege kuwa sehemu moja (Zero graizing).

Deni la ada ya kuzoa taka na jinsi ya kudaiwa

25 (1) Ada yoyote ya kuzoa taka inavyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi itakuwa ni deni kwa Halmashauri au wakala wake na inaweza kudaiwa kutoka kwenye kaya au mmiliki wa biashara kwa mujibu wa sheria.

(2) Madeni ya ada ya kuondoa taka ilioainishwa kwenye kifungu cha (1) cha Sheria Ndogo hii yatakusanywa kutoka kwa mmiliki kwa kumpelekea Hati ya madai kwa maandishi na iwapo atashindwa kulipa kwa muda wa siku 14 Halmashauari au mtu yeyote aliyeidhinishwa anaweza kufungua kesi ya jinai mahakamani au kukamata mali ya mdaiwa yenye dhamani ya kiasi anachodaiwa.

Mali iliyokamatwa kwa jinsi hii itauzwa kwa mnada wa hadhara iwapo mhusika hataikomboa ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu ilipokamatwa.

Shahada ya mahakama kuthibitisha usahihi wa maelezo yaliyotolewa

26 (1) Baada ya uthibitisho wa Mkurugenzi au afisa aliyeidhinishwa juu ya deni lenyewe na kuhakikisha kuwa mmiliki hajalipa licha ya kupelekewa madai, mahakama itathibitisha madai hayo kwa kutoa shahada/hati, na hivyo itakuwa hati ya idhini ya kutekeleza hukumu dhidi ya madai hayo kwa njia yeyote ile na itakuwa sawa na inayotolewa na mahakama hiyo kwenye kesi nyingine za jinai.

(2) Kila shahada inayopelekwa katika mahakama kama ilivyo kwenye Sheria Ndogo hizi itakuwa ni kielelezo cha kweli cha kuonyesha maelezo yaliyotolewa ni sahihi.

Kufutiwa leseni ya biashara

27 (1) Isipokuwa pale ambapo sheria andishi nyingine inaeleza vinginevyo, Mkurugenzi anaweza kufuta leseni ya biashara pale ambapo mmiliki mwenye biashara atakapo shindwa kuonyesha stakabadhi ya kulipia ada ya taka.

(2) Kabla ya kufuta leseni hiyo Halmashauri au afisa aliyeruhusiwa atatakiwa atoe ilani ya maandishi ya siku zisizopungua kumi na nne kueleza nia ya kufanya hivyo kwa kumtaka mhusika alipe ada hiyo mara moja.

Muda wa kulipa ada

28 Ada itatakiwa kulipwa ndani ya siku thelethini baada ya mmiliki, mpangaji au mfanya biashara kupata taarifa.

Wakala wa kukusanya ada na kuzoa taka

29 Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote kukusanya ada na au kuzoa taka na inaweza kuingia naye mkataba wa kufanya kazi za ukusanyaji na uzoaji taka ikiwa ni pamoja na kumpa uwezo wa kumpeleka mahakamani mtu yeyote anayeshindwa kulipa ada ya ukusanyaji au uzoaji taka kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Ilani ya kuondoa adha za taka

30 (1) Iwapo adha itaonekana mahali au karibu na makazi kwa sababu ya taka za biashara au taka za majumbani kutupwa eneo la makazi kwa makusudi, Halmashauri itampa ilani mmiliki au mkazi anayeishi kwenye nyumba hiyo na kumtaka aondoe adha hiyo kwa muda utakaotakiwa kwa maandishi na iwapo muda aliopewa katika ilani utamalizika, adha ikiwa inaendelea au kurudiwa atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Halmashauri inaweza kumtaka mmiliki au mkazi wa nyumba yoyote au mkazi kuondoa adha katika eneo lake. Endapo mmiliki atashindwa, Halmashauri inaweza kuondoa adha hiyo na mmiliki wa nyumba au biashara atalazimika kulipa gharama zote zilizotumiwa na Halmashauri kuondoa adha hiyo.

Usafi kwenye viwanja na maeneo yaliyo wazi

31 Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote au mmilki wa kiwanja chochote au sehemu ya kiwanja ambacho hakikuendelezwa au kuwa na mtu au mwenye kiwanja ambacho hakina mkazi au kuendelezwa kutupa mahali hapo kitu chochote kinachoudhi au kutupwa kwenye barabara au eneo lililo wazi kutoka nyumba yoyote ile iwe ni masalia ya vya vyakula, makombo au masalia ya vyakula vya mifugo au kinyesi au mzoga wa aina yoyote ile.

Uwakilishi katika uwajibikaji

32 (1) Kila mwenye nyumba ya makazi au nyumba ya biashara atawajibika kuwakilisha mmiliki chini ya Sheria Ndogo hizi kwa makosa atakayofanya mmiliki au mpangaji wa nyumba hiyo ya makazi au ya biashara.

(2) Afisa yeyote au wakala ambaye ameidhinishwa kwa kumtumia mwakilishi wa mamlaka hiyo iliyoiwakilishwa anaweza kwa wakati anaoona unafaa kufanya ukaguzi, uchunguzi au kukagua utekelezaji wa kazi katika eneo lolote lililopo chini ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Ada ya kutupa taka dampo

33 (1) Kutakuwepo na ada ya kutupa taka katika Dampo kuu la Halmashauri kwa kila wakala, taasisi za kijamii, taasisi zisizo za kiserikali na taasisi nyingine zozote ambazo zitajishughulisha na kuzoa na kutupa taka kadri itakavyopangwa na Halmashauri.

(2) Kwa kila wakala, taasisi za kijamii, taasisi zisizo za kiserikali na taasisi nyingine zozote ambazo zitajishughulisha na kuzoa na kutupa taka ambazo hazitakuwa na uwezo wa kukusanya na kupeleka takataka dampo kuu kwa vyombo na magari yao, watatozwa shilingi elfu kumi na tano (15,000/=) kwa tripu moja kama gharama za mafuta kwa Halmashauri.

(3) Taasisi zisizo za kiserikali, taasisi za kiserikali na mtu yeyote atakaye jishughulisha na uzoaji na utupaji taka ambaye atashindwa au kukataa kulipa ada ya utupaji taka,

atakuwa ametenda kosa na atatakiwa kulipa asilimia ishirini 20% zaidi ya ada kama adhabu.

(4) Kila wakala, taasisi za kijamii, taasisi zisizo za kiserikali na taasisi nyingine zozote ambazo zitajishughulisha na kuzoa na kutupa taka zitanunua na kutumia stakabadhi za Halmashauri zilizochapishwa kwa kazi hiyo. Kila kitabu cha stakabadhi kitakapoisha, wakala atawajibika kuilipa Halmashauri asilimia 6 (6%) ya makusanyo yote aliyokusanya kwa kitabu hicho.

Makosa na adhabu

34 (1) Mtu yeyote atakaye kataa au atakaye dharau au kushindwa kutekeleza Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na itakapothibitika atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote viwili kwa pamoja.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumtoza mvunjaji wa sheria ndogo hizi faini yake ya papo kwa papo kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini endapo mkosaji au mvunjaji atakiri kosa kwa kujaza fomu maalumu ambayo inapatikana katika Jedwali Na. 6 la Sheria Ndogo hizi.

(3) Mtuhumiwa atakuwa ana haki ya kukataa kosa kwa kwenda kujibu shitaka mahakamani, na endapo mahakama itamtia hatiani atalipa gharama zote za kuendesha shauri tangu atende kosa, na kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kwenda gerezani miezi kumi na mbili au vyote faini na kifungo.

(4) Baada ya kumaliza adhabu aliyopewa na kifungu cha *(2) na (3) vya Sheria Ndogo hii, mkosaji atawajibika kusafisha na kufanya marekebisho ya uharibifu alioufanya kadri halmashauri itakavyoona inafaa.

Adhabu ya jumla

35 Mtu yeyote atakayekiuka kifungu chochote cha Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na iwapo atapatikana na hatia kama hakuna adhabu maalum iliyoainishwa katika kifungu kilichokiukwa atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi sita jela au vyote kwa pamoja, faini na kifungo.

Wajibu wa mzabuni

36 (1) Taasisi zisizo za kiserikali, taasisi za kijamii (CBO's), tasasisi za kiserikali na mtu yeyote au Kampuni atakaye jishughulisha na uzoaji na utupaji taka zitafanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mji katika

mitaa au kata watakazopangiwa kupitia zabuni, zitawajibika au atawajibika kukusanya taka ngumu na kuzipeleka kwenye sehemu maalumu ya kukusanyia taka (collection point) au Dampo kuu, pia zitawajibika au atawajibika kukusanya ada za taka ngumu katika maeneo wanayotoa huduma.

(2) Taasisi zisizo za kiserikali, taasisi za kijamii (CBO's), taasisi za kiserikali na mtu yeyote au Kampuni atakaye jishughulisha na uzoaji na utupaji taka zitawajibika au atawajibika kuingia mkataba na Halmashauri wa kuendesha aina ya shughuli ya usafi wa mji au kudhibiti taka ngumu kama watakavyo elekezwa na Halmashauri.

Wajibu wa kamati za maendeleo

37 Kamati za maendeleo za kata zikisaidiwa na zile za mitaa zitahusika katika utekelezaji wa shughuli zote za usafi pamoja na maslahi ya vikosi kazi na Halmashauri.

Uhamasishaji wa kuzitambua sheria hizi

38 Halmashauri itawajibika kuhamasisha jamii, uundaji wa vikosi kazi na CBO's kuzitambua, kuzipa nguvu za kisheria na kuziwezesha kuanza kazi.

Utekelezaji wa sharia hizi

39 Utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi unaenda sambamba na utekelezaji wa sheria mama za kila sekta zinazohusu usafi wa mazingira.

JEDWALI

## *JEDWALI NA.1*

### ADA MBALIMBALI ZA HUDUMA ZA USAFI WA MAZINGIRA

***JEDWALI NA.1 –Ada za uzoaji taka ngumu***

| Na. | AINA YA BIASHARA | KANDA 'A' | KANDA 'B' | KANDA 'C' |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Maeneo ya kaya | 1,000/= | 1,000/= | 1,000/= |
| 2 | Tea room | 2,500/= | 2,500/= | 2,500/= |
| 3 | Café | 4,500/= | 3,000/= | 2,500/= |
| 4 | Ice cream/barafu | 5,000/= | 4,000/= | 2,500/= |
| 5 | Restaurant | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 6 | Nyumba za Wageni | 10,000/= | 8,000/= | 5,000/= |
| 7 | Dispensary (normal refuse) | 10,000/= | 8,000/= | 6,000/= |
| 8 | Health centre (normal refuse) | 12,000/= | 10,000/= | 8,000/= |
| 9 | Viwanda vidogo/garage | 5,000/= | 4,000/= | 3,000/= |
| 10 | Hotel: Vyumba 1-10 | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| | - Vyumba 11-20 | 30,000/= | 30,000/= | 30,000/= |
| | - Vyumba 21-30 | 40,000/= | 40,000/= | 40,000/= |
| | - Vyumba 31-40 | 45,000/= | 45,000/= | 45,000/= |
| | - Vyumba 41-50 | 60,000/= | 60,000/= | 60,000/= |
| | - Vyumba 61-70 | 80,000/= | 80,000/= | 80,000/= |
| | - Vyumba 71-80 | 90,000/= | 90,000/= | 90,000/= |
| | - Vyumba 81- 100 | 100,000/= | 100,000/= | 100,000/= |
| 11 | Maduka ya dawa muhimu | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 12 | Bucha | 8,000/= | 5,000/= | 5,000/= |
| 13 | Masoko kwa chumba (stals) | 5,000/= | 3,000/= | 2,000/= |
| 14 | Magenge | 2,000/= | 2,000/= | 2000/= |
| 15 | Wauza vyakula mitaani | 1,000/= | 1,000/= | 1,000/= |
| 16 | Magari ya mizigo (cargo) | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| 17 | Biashara ndogondogo | 1000/= | 1000/= | 1000/= |
| 18 | Dobi | 1,000/= | 1,000/= | 1,000/= |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 19 | Saloon/vinyozi | 5,000/= | 4,000/= | 3,000/= |
| 20 | Vituo vya mafuta | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| 21 | Wauza mikaa | 3,000/= | 3,000/= | 3,000/= |
| 22 | Maduka ya jumla | 15,000/= | 10,000/= | 8,000/= |
| 23 | Maduka ya vyakula (super markets) | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| 24 | Maduka ya Hardware | 25,000/= | 20,000/= | 10,000/= |
| 25 | Maduka ya rejareja | 10,000/= | 8,000/= | 5,000/= |
| 26 | Dry cleaner | 10,000/= | 10,000/= | 5,000/= |
| 27 | Radio service | 5,000/= | 4,000/= | 2,000/= |
| 28 | Sonara (g/smith) | 4,000/= | 3,000/= | 3,000/= |
| 29 | Laboratories | 8,000/= | 7,000/= | 5,000/= |
| 30 | Furniture/carpentry | 10,000/= | 5,000/= | 5,000/= |
| 31 | Video show | 5,000/= | 4,000/= | 3,000/= |
| 32 | Battery charge | 3,000/= | 3,000/= | 2,000/= |
| 33 | Refrigerate services | 3,000/= | 3,000/= | 3,000/= |
| 34 | Welding | 3,000/= | 3,000/= | 2,000/= |
| 35 | Plumbers | 4,000/= | 3,000/= | 2,000/= |
| 36 | Kuuza mapipa | 3,000/= | 3,000/= | 2,000/= |
| 37 | Scale services | 2,000/= | 2,000/= | 2,000/= |
| 38 | Posho mills | 20,000/= | 15,000/= | 10,000/= |
| 39 | Pombe shop | 5,000/= | 3,000/= | 2,000/= |
| 40 | Garments | 8,000/= | 6,000/= | 5,000/= |
| 41 | Wachoraji | 2,000/= | 2,000/= | 2,000/= |
| 42 | Soda (whole scale) | 15,000/= | 10,000/= | 8,000/= |
| 43 | Studio | 4,000/= | 4,000/= | 4,000/= |
| 44 | Spare parts | 8,000/= | 5,000/= | 3,000/= |
| 45 | Mafuta ya taa mitaani | 1,000/= | 1,000/= | 1,000/= |
| 46 | Karakana | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 47 | Bakeries | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| 48 | Kuuza magazeti | 1,000/= | 1,000/= | 1,000/= |
| 49 | Computer services | 5,000/= | 3,000/= | 2,000/= |
| 50 | Godowns | 8,000/= | 5,000/= | 5,000/= |
| 51 | Stores | 5,000/= | 3,000/= | 2,000/= |
| 52 | Water kiosks | 1,000/= | 1,000/= | 1,000/= |
| 53 | Fish maws | 1,000/= | 1,000/= | 1,000/= |
| 54 | Mabasi ya express | 2,000/= | 2,000/= | 2,000/= |
| 55 | Night club | 20,000/= | 15,000/= | 10,000/= |
| 56 | Makanisa | 5,000/= | 5,000/= | 5,000/= |
| 57 | Miskiti | 5,000/= | 5,000/= | 5,000/= |
| 58 | Maduka makubwa ya dawa(Pharmacy) | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| 59 | Grocery | 10,000/= | 8,000/= | 6,000/= |
| 60 | Baa | 15,000/= | 10,000/= | 8,000/= |
| 61 | Waosha magari | 10,000/= | 8,000/= | 6,000/= |
| 62 | Shule za msingi | 5,000/= | 5,000/= | 5,000/= |
| 63 | Shule za sekondari | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 64 | Viwanda (taka nzito kwa tani) | 5,000/= | 5,000/= | 5,000/= |
| 65 | Viwanda (taka nyepesi kwa trip) | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| | Hospitali | | | |
| | Vitanda 1-10 | 10,000/= | 10,000/= | 10,000/= |
| | Vitanda 11-20 | 12,000/= | 12,000/= | 12,000/= |
| | Vitanda 21-30 | 15,000/= | 15,000/= | 15,000/= |
| | Vitanda 31-40 | 20,000/= | 20,000/= | 20,000/= |
| | Vitanda 41-50 | 25,000/= | 25,000/= | 25,000/= |
| | Vitanda 61-70 | 30,000/= | 30,000/= | 30,000/= |
| | Vitanda 71-80 | 40,000/= | 40,000/= | 40,000/= |
| | Vitanda 81-90 | 60,000/= | 60,000/= | 60,000/= |
| | Vitanda 91-100 | 80,000/= | 80,000/= | 80,000/= |
| | Vitanda 101 na kuendelea | 100,000/= | 100,000/= | 100,000/= |

***JEDWALI NA.2 . Ada ya unyonyaji majitaka***

| **SN** | **AINA YA BIASHARA** | **KIASI KWA SAFARI MOJA (trip)** |
|---|---|---|
| **1** | **Nyumba ya kuishi** | **35,000.00** |
| **2** | **Taasisi** | **50,000.00** |
| **3** | **Viwanda** | **100,000.00** |
| **4** | **Kukodi gari nje ya Manispaa** | **500,000.00 kwa siku bila gharama za mafuta** |

***JEDWALI NA. 3. ADA YA UKAGUZI***

(i) Hoteli…………………………………… Shs. 100,000/- kwa mwaka
(ii) Migahawa/baa………………….... Shs. 50,000/- kwa mwaka
(iii) Nyumba za kulala wageni…….. Shs. 50,000/- kwa mwaka
(iv) Viwanda…………………………….. Shs. 100,000/- kwa mwaka
(v) Biashara nyinginezo……………. Shs. 10,000/- kwa mwaka
(vi) Ukaguzi wa dharura……………. Shs. 20,000/- kwa mwaka
(vii) Viwanda vya matofari……….. . Shs. 50,000/- kwa mwaka

***JEDWALI NA 4* ADA *YA KUPULIZIA WADUDU***

(i) Ada ya kupulizia dawa ya wadudu (Fumigation) ambayo itafanywa na Halmashauri shs. 5000/- kwa mita za mraba za eneo (per square meter)
(ii) Ada ya usimamizi wa kunyunyizia dawa ya wadudu unaofanywa na watu binafsi shs. 5,000/- kwa kazi.

***JEDWALI NA* 5 *ADA YA KUPIMA WAHUDUMU***

(I) Kila mhudumu wa nyumba ya kulala wageni, Hoteli; Mgahawa, café, maduka ya nyama (bucha), wauza maziwa, viwanda, maduka ya vyakula, Muuza vyakula vilivyopikwa au kukaangwa anawajibika, kujisajili kwa Halmashauri ili kubainisha usalama wa Afya yake kabla ya kutoa huduma kwa wateja kama inavyoelekezwa na sheria ya Afya ya Jamii namba 1 ya Mwaka 2009. Kila mhudumu atapimwa Afya yake kila baada ya miezi sita (6) na atawajibika kulipa shilingi 5,000.00 kila anapopimwa.

## JEDWALI NA 6

## SHERIA NDOGO ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA MWAKA 2013.

## HATI YA KUKIRI KOSA

**(Chini ya kifungu cha 36 (2))**

Mimi…………………………………….. Nakiri mbele ya…………..……Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwamba mnamo tarehe……… ya mwezi wa………………….mwaka………. nilikutwa na kosa kwa kukiuka masharti ya kifungu cha ……………….. Cha Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za mwaka 2013, Nipo tayari kulipa kiasi cha faini ninachodaiwa kama kifungu cha 35 kinavyoeleza.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Tarehe…………………………….. Sahihi…………………………